



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AGIZO LA UTENDAJI

No. 2020-28

Kurejeshwa kwa huduma ya maji katika makazi ambayo watu wanaishi wakati wa Mulipuko wa janga la COVID-19

Virusi vya corona (COVID-19) ni ugonjwa wa upumuaji ambao huleta matokeo ya umahututi au kifo. Husababishwa na aina mpya ya virusi vya corona ambavyo hapo awali havikupatikana kwa wanadamu na ni rahisi kuenea kutoka kwa mtu hadi mwingine. Kwa sasa hakuna chanjo au matibabu yaliyoidhinishwa kwa ugonjwa huu.

Mnamo mwezi wa Tatu tarehe 10, 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Michigan ilitambua kesi mbili za kwanza zinazohusika na ugonjwa wa COVID-19 ndani ya Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa agizo la mtendaji 2020-4. Agizo hili lilitangaza hali ya hatari katiko jimbo/mkoa wote lote chini ya sehemu 1 cha kifungu cha 5 cha Katiba ya Michigan ya 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, kama ilivyorekebishwa, MCL 30.401-.421, na Nguvu za Dharura za Gavana 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebishwa, MCL 10.31-.33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura inampatia gavana nguvu na majukumu makubwa ya “Kukabiliana na hatari kwa jimbo/mkoa huu au watu wa jimbo/mkoa huu wanaokabiliwa na janga au dharura”, ambayo gavana anaweza kutekeleza kupitia maagizo ya mtendaji, matangazo, na maelekezo ya moja kwa moja yaliyo na nguvu na athari za sheria.” MCL 30.403(1)-(2). Vivyo hivyo Sheria ya Nguvu za Dharura za Ganava 1945, hutoa kwamba, baada ya kutangaza hali ya hatari, “gavana anaweza kutangaza agizo la busara, sheria, na kanuni kama anavyoona ni muhimu kulinda maisha na mali au kuleta hali ya dharura ndani ya eneo lililoathiriwa.” MCL 10.31(1)

Ili kupunguza kuenea kwa COVID-19, kulinda afya ya umma na kuepuka vifo visivyo vya lazima ni muhimu kwa wakazi wote wa Michigan kubaki manyumbani mwao au popote pale wanapoishi kwa kiwango kubwa iwezekanavyo na kuosha mikono yao vizuri na mara kwa mara. Sasa hivi zaidi ya hapo zamani, utoaji wa maji safi kwa makazi ni muhimu kwa afya ya binadamu, afya ya umma, na usalama wa jimbo hili. Vivyo hivyo, huduma nyingi za maji tayari zimesimamisha kufungwa kwa maji kwa wakati huu mgumu. Kutokana na uhitaji muhimu wa kuhakikisha kuwa wakaazi wa Michigan wanapata maji safi nyumbani wakati wa janga la COVID-19, ni sahihi na lazima kuhitaji marejesho ya maji safi katika Jimbo lote la Michigan kwa wakati huu wa dharura. Na kwa sababu ni muhimu pia kwa serikali ya jimbo kuwa na habari za kisasa na sahihi kuhusu upatikanaji wa maji safi, ni sahihi na lazima kuhitajika kwa wanavifaa wa maji wa umma kuripoti kuhusu hali ya huduma ya maji ndani ya maeneo yao ya huduma.

Kwa kupitia katiba ya Michigan ya 1963 na sheria ya Michigan, ninaamuru yafuatayo:


1. Usambazaji wa maji ya umma lazima urekebishe huduma ya maji kwa makazi yote ambayo wakazi wanaishi ambapo huduma ya maji imefungwa kwa sababu ya malipo kutolipiwa, ili mradi huduma ya maji ya umma haina sababu ya kuamini kwamba kuunganishwa tena kunaweza kusababisha hatari kwa afya ya umma (kwa mfano, kwa sababu maji kuwa chafu na hatari kwa wakazi). kuwezesha urejesho wa huduma ya maji, usambazaji wa maji ya umma lazima bidii wa mara moja ufanye nguvu ya kudhibitisha ni makazi gani kati ya maeneo yao ya huduma haiza huduma ya maji. Kwa madhumuni ya agizo hili, “eneo la huduma ya maji” linamaanisha eneo ambalo usambazaji wa maji ya umma unakusanya malipo kwa huduma ya maji.
2. Ikiwa usambazaji wa maji ya umma utaamua kuwa makazi yoyote katika eneo lake la huduma imefungiwa huduma ya maji kwa sababu lolote ile isipokuwa ya malipo au uhusiano huo unaweza kusababisha hatari kwa afya ya umma, lazima ifanye juhudi nzuri ya kurekebisha hali kama hiyo na kurejesha huduma ya maji kwa makazi kwa haraka iwezekanavyo.
3. Kwa haraka iwezekanavyo na si baada ya April 12, 2020, usambazaji wote wa maji ya umma ambao ulifunga maji kama dawa ya kutolipiwa katika mwaka uliopita lazima waripoti katika Kituo cha Operesheni cha Dharura za Jimbo kuhusu upatikanaji wa maji katika maeneo yao ya huduma. Ripoti lazima iwe pamoja na:
 - (a) Akaunti ya juhudi gani zimefanywa ili kuamua ni makazi gani kati ya eneo la huduma ya usambazaji maji haina huduma ya maji
 - (b) Idadi ya wakazi waliomo katika eneo la huduma ya usambazaji wa maji ya umma ambayo haina huduma ya maji kwa sababu ya kutolipiwa.
 - (c) Idadi ya wakazi waliomo katika eneo la huduma ya usambazaji wa maji ya umma ambalo halina huduma ya maji kwa matokeo ya kufungwa kutokana na kutokulipiwa.
 - (d) Udhhibitisho, ikiwa ni sahihi, kwamba juhudi bora zimetetelezwa ili kuamua ni makazi gani katika eneo la huduma hayana huduma ya maji; kwamba, kwa ufahamu bora wa usambazaji wa maji ya umma, hakuna makazi ya waakazi ambayo maji yatafungwa kutokana na kutokulipiwa; ni kwamba usambazaji wa maji ya umma umeunganisha huduma ya maji kwa makazi yote yaliyo na wakaaji ambayo yanaweza kuunganishwa tena bila kuunda hatari kwa afya ya umma; na kwamba usambazaji wa maji kwa umma umetumia juhudi nzuri ya kurekebisha hali ambazo zinazuia kuunganishwa tena kutokana na hatari kwa afya ya umma.
4. Kama usambazaji wa maji ya umma utawasilisha ripoti chini ya kifungu cha 3 cha agizo hili ambalo halifikii mahitaji yote yaliyoelezwa katika kifungu cha 3, basi usambazaji wa maji ya umma lazima uwasilishe ripoti ya nyongeza kila siku 30 hadi itakapowasilisha ripoti itakayokamilisha mahitaji yote ya kifungu cha 3.

5. Hakuna chochote katikat agizo hili kinachomsihi mkazi kutolipia huduma ya maji, kinachozuia usambazaji wa maji ya umma kuchaji mteja yeyote malipo ya huduma ya maji, au kupunguza kiasi ambacho mkazi anadaiwa kwa sababu ya usambazaji wa maji ya umma.
6. Agizo hili linafaaa kuimarishwa kwa mara moja na kuendelea hadi hali ya dharura chini ya kifungu cha 3 cha Agizo la Utendaji 2020-4 litakapoondolewa.

Imetolewa chini ya idhini yangu na Muhuri Mkuu wa Jimbo la Michigan.

Tarehe: Machi 28, 2020

Muda: 7:09 jioni



GRETCHEN WHITMER
GAVANA

Kutoka kwa Gavana:

KATIBU WA SERIKALI